

YAKINI

 Asante, ndugu. Asante, Ndugu Hoekstra.

Habari za jioni, kwa Houston. Bila shaka nachukulia haya kuwa ni majaliwa makuu, ya kuwa hapa tena usiku wa leo huku Houston. Imekuwa ni miaka mingi tangu nilipokuwa na majaliwa ya kuwa hapa. Nami nimekuwa nikiketi, nikisikiliza usiku wa leo kila mmoja wa wahubiri hawa.

² Basi hivi majuzi, wakati nilipokuwa na matayarisho yaliyowekwa kwa ajili ya jambo lingine, mahali pengine, nami nilijua ya kwamba watoto hao walikuwa wanakabiliwa na mauti, niliwaza, “Kama jambo fulani lingetokea kwa watoto hao, kamwe singeweza kujisamehe,” kwa kutokuja hapa kutoa maoni yangu na kufanya yote niliyoweza, kumsaidia mama huyu na baba, na watoto hawa, na kufanya yote niwezayo kwa ajili ya kuyaokoa maisha yao.

³ Nayo Houston ina... ni mahali pa kumbukumbu kwangu mimi. Inashikilia kumbukumbu nyingi kubwa ambazo nimehifadhi tangu nilipopatembelea mahali hapa kwa mara ya kwanza miaka mingi iliyopita, hapa kwenye M̄biu Ya Imani, Ndugu Kidson, na halafu hapa chini kwenye jumba la mikutano wakati nilipokuwa hapa pamoja na Ndugu Raymond Richey na wahudumu wa mjini.

⁴ Ndipo basi, hakika, Bw. Ayers, Bw. Kipperman, ule usiku ambaao kamera ilithibitisha ya kwamba sikuwa nikisema uongo wowote. Ilikuwa ni Kweli. Ndipo wakati jicho la kimitambo la kamera liliposhika lile ono la ninii... ama, sio ono; uhalisi. Yule Kristo tunayemhubiri na kumpenda sana, alikuwa pamoja nasi. Aliahidi kuwa pamoja nasi, nayo kamera ikapiga picha Yake. Mara nyingi nimesema, nyakati zilizopita, kwamba—kwamba ningeiona Nuru hiyo wakati wote. Lakini wakati mwingeine watu wangekuwa na shaka kidogo juu Yake, ambalo ungeweza kuamini wangeweza kuwa hivyo, lakini usiku huo ililithibitisha. Hiyo ilikuwa ndiyo mara ya kwanza ilipopata kupigwa picha.

⁵ Tangu wakati huo, imepigwa picha mara kadhaa. Huko Ujerumani hivi majuzi tu, ikishuka, wakati upako ulipokuwako, na wakati iliporudi tena. Na mambo hayo si ya kumtukuza mwanadamu fulani, bali ni kuthibitisha Uwepo wa Yesu Kristo mionganoni mwa watu Wake.

⁶ Nasi tunaamini ya kwamba Bwana Yesu yuyo huyo yupo hapa usiku wa leo, kutusaidia katika kesi hii. Nami ninaamini anaijali hiyo zaidi ya vile tungeweza kuwa. Nami bila shaka ninawahurumia wazazi wa watoto hawa, na bega kwa bega pamoja na kila mwanamume na mwanamke anayejaribu kuwaokoa na hatari hii kubwa.

⁷ Pia, sasa, nasikia ya kwamba huu si mkutano wa uamsho, bali ni m—mfululizo tu wa mikutano ya maombi yanayofanywa kwa ajili ya nafsi hizi zilizo katika vivuli vya mauti. Na kwa hiyo nimechelewa. Sitazungumza muda mrefu sana.

⁸ Lakini ningetaka kuchukua somo, ama fungu la maneno, hasa, kutoka kwenye somo ambalo ningetaka kusoma katika mahali pawili katika Maandiko. Nanyi mlion na Biblia, kama mngeweza kufungua pamoja nami kwa muda mfupi tu, kwenye Kitabu cha Wafilipi, mlango wa kwanza, na kifungu cha 20 cha mlango wa kwanza wa Wafilipi.

*Kama vile nilivyotazamia sana, na kutumaini,
kwamba sitaaibika kamwe, bali...kwa uthabiti
wote, kama sikuzote na sasa vivyo hivyo Kristo
ataadhimishwa katika mwili wangu, ikiwa kwa...
maisha, au...mauti.*

⁹ Halafu basi katika, pia, katika Kitabu cha Matendo, mlango wa 2 na kifungu cha 30. Huenda nikasoma cha 25 hadi cha 30.

*Maana Daudi alinena habari zake, kwa kuwa
nalimwona Bwana mbele yangu siku zote, kwa kuwa
yuko upande wa mkono wangu wa kuume, nisitikisike.*

*Kwa hiyo moyo wangu ukapendezewa, ulimi wangu
ukafurahi, tena mwili wangu nao utakaa katika
matumaini.*

*Kwa kuwa sitaiacha roho yangu katika kuzimu; wala
sitamtoa Mtakatifu wako aone uharibifu.*

*Umenijuvisha njia ya uzima; utanijaza furaha kwa uso
wako.*

*Waume na ndugu zangu, mniwie radhi, niseme nanyi
kwa ujasiri habari za baba yetu mkuu Daudi, ya kuwa
alifariki akazikwa, na kaburi lake liko kwetu hata leo.*

*Basi kwa kuwa ni nabii, akijua ya kuwa Mungu
amemwapia kwa kiapo, ya kwamba katika uzao wa
viuno vyake kwa habari za mwili, atamwinua Kristo
aketi katika kitie chake cha enzi;*

*Yeye mwenyewe akitangulia kuyaona haya, alitaja
habari za kufufuka kwake Kristo, ya kwamba roho
yake haikuachwa kuzimu, wala mwili wake haukuona
uharibifu.*

¹⁰ Na tuinamishe vichwa vyetu kidogo tu kwa ajili ya maombi.

¹¹ Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru Wewe kwa ajili
ya neema. Na hiyo ni kweli, Bwana, ndiyo sababu ya sisi
kuwa hapa usiku wa leo, ni kuomba rehemba. Tusingeomba hili
ikiwa hatukuwa na imani kuamini ya kwamba tungepewa. Watu
wameruka kote nchini, na maombi yanapaa juu kila mahali,
Kwako, kwamba maisha ya hawa amba tunawaombea kwa

dhati usiku wa leo yaokolewe. Bwana, tungeomba nguvu kwa ajili ya mama na baba wa vijana hawa.

¹² Na kama tunavyoolewa, kwamba, kijana mwanamume huyu ameyatoa maisha yake Kwako na anataka kukutumikia. Na kama tulivyomsikia mmoja wa wanenaji akisema, ya kwamba, ye ye alitaka kuwa mhudumu wa Injili, ninaomba, Mungu, ya kwamba utaijalia nafasi hii kwa jamaa huyu mdogo.

¹³ Tusamehe dhambi zetu, isafishe miyo yetu na mawazo maovu, na chocote kinachoweza kuwa njiani mwetu ambacho kingezuia maombi yetu yasjibiwie kwa ajili ya watu hawa.

¹⁴ Kama vile tumelisoma Neno Lako, tunajua ya kwamba mbingu na nchi pia zitapita bali Neno Lako halitashindwa. Tunaomba ya kwamba Wewe utatuongezea, kwa Roho Mtakatifu, muktadha ambao ungechukua, ambao ungekuwa ni mapenzi Yako ya Kiungu katika kesi hii sasa, kama tulivyomsikia wakili na wengi wakizungumza. Nasi tunaomba ya kwamba tutapata tu la kufanya baada ya haya, kwamba hatua yetu inayofuata ya kufanya ni ipi. Bwana, tupo hapa kuitekeleza. Tujulishe, Bwana, kuititia Neno Lako. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Mwana Wako, Bwana Yesu Kristo. Amina.

¹⁵ Huku nikisoma vifungu hivi vichache, na ninatambua fursa hii ni kuu, kwa sababu ya shughuli yake. Ningewazia, wakati niliposikia na kupata telegramu ya mama huyo, “Vipi kama huyo alikuwa ni mwanangu aliyeketi kwenye vurugu hiyo, ama binti yangu?” Na mimi... Tunataka kuweka kila kitu tuwezacho kwa hilo.

¹⁶ Ndipo huenda wengine wakasema, “Vema, hiyo ilikuwa ni sehemu ndogo sana ya Neno, uliyosoma, Ndugu Branham.” Vema, huenda hiyo ikawa ni kweli, pia. Lakini, unaona, si u-ukubwa, ama wingi wa maneno. Ni kile linalomaanisha. Ni—ni ninii tu... Kile lilicho, ni ahadi ya Mungu.

¹⁷ Nami ninataka kutoa kutoka kwenye hili usiku huu, kutoka kwenye somo hili usiku wa leo, ama somo kutoka kwenye hili: *Yakini*.

¹⁸ Nimelichagua somo hili, muda mfupi uliopita, nikiwa nimeketi kwenye chumba changu cha hoteli, kwa sababu nafikiri ya kwamba sasa tunahitaji jambo la hakika, yakini fulani tunayoweza kushikilia na kujua ya kwamba ni kweli. Katika saa muhimu kama hii, lazima tuwe na jambo ambalo tuna hakika, lililo kweli, jambo ambalo tunaweza kushikilia, kujua iwapo, jinsi ambavyo kesi inaendelea.

¹⁹ Sasa, kulingana na—na Webster, *yakini*, lenyewe, ni “lisilo na kikomo katika nguvu zake,” na kimsingi ni “mkataa.” Na *mkataa* ni “amina.” Ni *yakini*. Kwa vile ni... Hiyo ni mwisho. Hiyo ni kila kitu.

²⁰ Sasa, kila mafanikio makuu ambayo yamekuwamo ulimwenguni, yameambatanishwa na namna fulani ya yakini. Huwezi kufanya lolote pasipokuwa na kitu ambacho unaweza kushikilia.

²¹ Kijana mwanamume anapoenda kufunga ndoa na kijana mwanamke, hana budi kujuu tabia ya kijana mwanamke huyu. Ama kijana mwanamke hana budi kujuu tabia ya kijana mwanamume, kitu ambacho anaweza kushikilia. "Mwanamume huyu atakuwa mtu wa haki? Atakuwa mume mzuri kwangu?" "Mwanamke huyu atanipa, maishani, yale mimi—yale ninayotarajia kutoka kwake, uaminifu na kadhalika?" Halafu basi hapana budi pawe ni mahali fulani wanapoweza kuwekea msingi nadhiri za—zao, wakijua ya kwamba kuna kitu fulani kitakachoshikilia. Na hiyo ndiyo sababu tunawaleta kanisani, na kwenye Neno la Mungu, kuifunganisha yakini hii.

²² Sasa, Paulo hapa, kama tunavyoona, alikuwa na yakini aliyoshikilia, maisha yake yote, baada ya wongofu wake, hiyo ilikuwa ni: maisha yenye msingi wa Kristo! Na ni mahali pa jinsi gani pa kuweka yakini: maisha yenye msingi wa Kristo! Yalikuwa ni maisha tofauti na yale aliyokuwa ameishi wakati mmoja, kwa kuwa alisema, "Maisha ninayoishi sasa," ambayo yalikuwa ni tofauti na yale aliyokuwa ameishi.

²³ Basi ilifikia wakati ambapo Paulo alipata tukio hili lililomfikisha kwenye uamuhi huu. Kwa kuwa, Paulo alikuwa mtu mkuu mashuhuri, mionganii mwa Wayahudi, na mwa—mwanatheolojia mashuhuri, bali hakuwa na uhakika sana na msimamo wake. Bali siku moja, akishuka kwenda Dameski, Nuru, Nguzo ya Moto, ilishuka kutoka Mbinguni. Naye Paulo, akiwa ni Myahudi, alifahamu kwamba Nuru hii, Nguzo ya Moto, ilikuwa ndiyo Kitu ambacho kilikuwa, Mungu ambaye alikuwa amewaongoza watu wake kutoka Misri. Walikuwa wameifuata Nguzo hii ya Moto. Kwa hiyo, akiwa ni Myahudi, alimwambia, upesi, "Bwana, U Nani Wewe?" Yeye alimfahamu kama "Bwana," lakini, "U Nani Wewe?"

²⁴ Ndipo Sauti ikatoka kwenye hiyo Nguzo ya Moto, "Mimi ni Yesu, na ni vigumu kwako kupiga teke michokoo." Tangu wakati huo na kuendelea, Paulo alijua ya kwamba Yehova wa Agano la Kale alikuwa ni Yesu wa lile Jipy. Naye alikuwa na kitu ambacho angeweza kushikilia, na hivyo ndivyo angeweza kuandika kile Kitabu mashuhuri cha Waebria.

²⁵ Sasa, ikiwa wewe, ikiwa katika maisha yako una yakini, unafanya mambo usingeweza kufanya kwa kawaida, hasa ikiwa una maisha yenye msingi wa Mungu. Maisha yenye msingi wa Mungu humfanya mtu kufanya mambo ambayo kwa kawaida wasinge yafanya; ya kipekee sana, ya tofauti. Ni kwa nini maisha ya Kikristo ni ya kipekee sana na ya tofauti? Ni kwa sababu

kwamba wanaliangalia Neno la Mungu, ambalo karibu ni la kigeni kwa ulimwengu siku hizi.

²⁶ Sasa, tunayo makanisa, na tunayo madhehebu, na tunayo dini, loo, nyingi sana, kote ulimwenguni.

²⁷ Katika mara zangu saba kuuzunguka, tangu nilipokuwa hapa Houston pamoja nanyi, nimekusanya maarifa mengi juu ya miungu na dini za ulimwengu huu. Bali hilo silo ninalozungumzia.

²⁸ Ninazungumza juu ya yakini, iliyowiana na Kristo. Ndipo, inakufanya m—mtu wa kipekee. Unafanya mambo ya kipekee. Kuwaza kwako kwa jumla ni tofauti na mawazo uliyowaza wakati mmoja, kwa sababu umepata kitu fulani, kwamba umetia nanga imani katika Mtu fulani aliyeumba mbingu na nchi, kwamba, Neno Lake Lenyewe ni umbaji, Mungu Yule aliyenena ulimwengu ukawepo, wala hakuna kitu kigumu kupita kiasi Kwake. Kwa hiyo linakufanya muumba, wewe mwenyewe, kwa sababu unayachukua Maneno Yake. Nalo neno ni wazo lililotamkwa.

²⁹ Sasa, Paulo alikuwa ameingia katika hali hiyo, kufikia ambapo yeye hakuwa—hakuwa na ujuzi wa kithiolojia, kwa jumla, bali alikuwa na ushahidi wa kibinagsi. Alikuwa amekutana na Mungu, na kujua ya kwamba aliitwa na Mungu. Na—na hakuna mtu aliypaswa kumwambia lolote kulihu. Alikuwa na uhakika kabisa ya kwamba Mungu angali alibaki Mungu. Laiti ulimwengu ungalifanya tu hilo!

³⁰ Basi laiti kundi hili usiku wa leo, linaloketi hapa, lingeweza kukumbuka tu ya kwamba Mungu angali ni Mungu! Yeye anaweza tu kujibu katika kesi hii kama anavyoweza katika kisa cha uponyaji wa Kiungu ama chochote kingine. Yeye angali ni Mungu. Basi laiti tungaliweza kujenga matumaini yetu, sio tu matumaini yetu, bali wa—wazo la haki, juu ya kile Yeye asemacho! Nasi tunajua kwamba Hilo ni Kweli.

³¹ Nao watu wanatenda kiajabu. Wanaonekana kusahau tu kuhusu upande ule hasi maana wamepata yakini, kwa sababu ni Neno la Mungu. Yesu alisema, “Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitashindwa.” Kwa hiyo kama tunalo Neno la ahadi, basi hakuna kushindwa Kwake. Haliwezi kushindwa.

³² Kwa hiyo ni—ninaamini ya kwamba hilo ndilo mikutano hii ya maombi hapa, wa—watu wa kidini wa Houston, wanavutiwa nalo, maisha ya binadamu. Na hiyo ndiyo sababu ya sisi kukusanyika hapa, ni kuninii—ni kuita nguvu ambazo zimepita sheria zote zilizobuniwa na wanadamu na nguvu, kitu fulani, Yeye awezaye kubadilisha miyo ya wanadamu, kama alivyomfanya Farao huko Misri. Na Yeye ni—Yeye ni Mungu. Nasi hatuna budi kuacha sasa kuangalia u—upande hasi, na tuanze kuangalia upande chanya.

³³ Na kabla hujaweza kuwa na imani, inakubidi kuwa na kitu fulani cha kuamini. Na ni kitu gani zaidi unachoweza kuitegemeza imani kuliko inavyoweza katika Neno la Mungu aliye hai, ambalo limeumba, nguvu za Mwenyezi? Ni kitu gani zaidi tungeweza kuwekea matumaini yetu? Kwa hiyo inakufanya uonekane tofauti, utende tofauti. Unamtazamia Mungu kuitimiza ahadi Yake. Na wakati matatizo yanapoinuka, kama tuliyo nayo sasa, Hilo ni nanga. Ni kitu fulani ambacho—ambacho hukushikilia, kitu ambacho umefungiwa kwake. Ni ahadi ambayo tumefungwa kwake, ndivyo liliyvo Neno la Mungu.

³⁴ Kama tu vile nanga ilivyvo yakini kwa meli, katika wakati wa tufani. Meli inaweza kuwa ikiabiri baharini. Nanga iko huko mbele. Ni ninii... Imetulia. Ninyi watu hapa Houston, mkiwa karibu sana na bahari, huona meli zikiingia.

³⁵ Basi kwa nini kubeba uzito huu wa ziada wa nanga hii kubwa mno? Lakini, mnaona, tufani zinapokuja, tu—tufani zinazochafuka ambazo hupasua bahari, na zingeweza kukirusha chombo ufukoni mahali fulani, na kukivunja vipandevipande, ama kukipindua katika maji yenye kina kifupi; inaingia kwenye maji ya kilindi, na kuitumbukiza nanga hii kubwa, kubwa mno, ambayo imetengenezwa hivi kwamba itajikokota chini ya bahari mpaka itie nanga juu ya mlima fulani usioonekana. Basi acha hizo tufani zivume zikitaka; ina yakini. Nanga inashikilia mahali fulani huko, bali i—imefungwa vizuri. Basi huku meli na mawimbi yakiigongagonga kote hiyo meli, inayo yakini, kwa sababu imefungwa.

³⁶ Na hivyo ndivyo mtu alivyo wakati amefunganishwa na Kristo na kwa Neno Lake, naye analiamini. Kuna yakini hapo, kitu fulani ambacho humshikilia.

³⁷ Yakini ni kama ile nyota ya kaskazini wakati umepotea. Wakati wewe—wakati umepoteza mwelekeo wako, nawe unataka kupata njia yako ya kurudi, nyota ya kaskazini ndiyo yakini. Sasa, kuna nyota zingine, bali zinazunguka pamoja na ulimwengu. Wakati ulimwengu unapozizinguka, ninii... unageuka mbali nazo. Na ninii... Mwajua, nyota ile ile ya asubuhi ndiyo nyota ya jioni pia, kwa sababu ulimwengu ulizunguka tu. Bali kuna nyota moja ambayo haisogeji, nayo imewekwa papo hapo katikati ya dunia. Na kwa hiyo ninii... Ni—ni nyota ya uhakika. Kama unaijua nyota ya kaskazini, daima unaweza kujua unakoenda. Lakini, loo, hapo ni wakati mtu amepotea, na hajui aeleeke wapi.

³⁸ Sasa, ninaijua Nyota moja. Loo, Hiyo ni zaidi ya nyota ya kaskazini. Na kufungwa na kuona Uwepo Wake, haijalishi umepotea namna gani ama mahali ulipo, unaweza kuipata njia yako ya kurudi kwa uongozi Wake, hilo ni Neno Lake. Ndiyo njia ya kutoka kwenye matatizo yote. Ndiyo njia ya kupata amani.

Ndiyo njia ya mafanikio. Ndiyo njia ya Uzima, yenyewe, ni kuifuata Nyota hii, Bwana Yesu. Na sasa, kama umefunganishwa kwenye Nyota hiyo, Roho Mtakatifu ndiye Dira ambayo itaelekeza tu kwenye hiyo Nyota. Ninii Takatifu . . .

³⁹ Dira, imetiwa sumaku ilekeze kwenye hiyo ncha ya kaskazini. Na njia pekee, haijalishi uko katika msitu kiasi gani, ama jinsi vichaka vilivyo vinene kukuzunguka, ama jinsi kulivyo na ukungu baharini, mkono huo wa dira, unaweza kuuzungusha vyovyyote utakavyo, nao utageuka moja kwa moja urudi na kuelekeza kwenye nyota ya kaskazini.

⁴⁰ Basi wakati tukiwa katika shida, na tunamtumainia Kristo, kuna jambo moja la hakika: Roho Mtakatifu atatuelekeza kwenye Neno ambalo litatuongoza hadi kwenye Nyota ya Kaskazini, na kuleta kila kitu tunachohitaji. Yeye ndiye Yakini yetu.

⁴¹ Kwa mtu aliyepotea nyikani, dira ndicho kitu kinachomwongoza atoke nje. Tunapokuwa katika shida, kuna jambo moja tu; ni la hakika tu kama nyota ya kaskazini. Mradi tu ulimwengu umesimama mahali pake, na unazunguka, nyota ya kaskazini itabaki mahali pake.

⁴² Na mradi tu kuna Umilele, Kristo daima atakuwa ni Mwokozi, na njia ya kutoka katika kila tatizo, kila tofauti, kila jaribio, kila kitu. Na kwa hiyo sisi—sisi, tunapofungamanishwa Kwake, hatuvurugiki na kuchanganyikiwa kama ulimwengu ufanyakavyo, “Ati, loo, tutafanya nini juu ya jambo *hili*? Tutafanya nini juu ya jambo *lile*?” Tunaonekana kana kwamba hata hatujatiwa nanga. Bali mtu ambaye ametia nanga nafsi yake katika Kristo Yesu, tumaini lake pale, akijua ya kwamba anapomwomba Baba lolote katika Jina Lake, “Yesu alisema, ‘Nitalifanya.’” Hilo latosha.

⁴³ Hilo—hilo linatosha. Ni amina. Ni yakini. Ni mkataa. Yesu aliposema, “Ombeni Baba lolote katika Jina Langu, nitalijalia,” sasa, huo ni mkataa. Jambo ndilo hilo. “Lolote mtakalo, mwombapo, aminini ya kwamba mtalipokea, nalo litakuwa lenu.” Hilo latosha. Hakuna lingine, mnaona, ikiwa kweli tumetiwa nanga na tunaliamini, na tumemfanya Yeye Yakini yetu. Maana, Yeye hufanya. Yeye ni Yakini inayotuondoa kwenye hofu yote. Hakuna hofu wakati umefungiwa kabisa kwenye ule Mwamba wa Kale.

⁴⁴ Hakuna hofu kwa baharia, jinsi meli inavyoshambuliwa kwa nguvu na mawimbi, mradi tu hiyo nanga imeshikilia juu ya ule mlima huko. Mbona, hakika. Anajua meli itaelea juu. Haiendi kugongana na mwamba mahali fulani. Haitaingia kwenye maji fulani yenyе kina kifupi na kupindulisha, kwa sababu ina yakini ambayo imetiwa nanga juu ya mlima fulani.

⁴⁵ Basi hapo mtu anapoweza kuomba maombi ya imani, na kuitia nanga nafsi yake huko kwenye Neno la Mungu, ambako,

“mbingu zote na nchi zitapita, bali Neno hilo haliwezi,” hakuna hofu. Acheni waje, waseme lolote wanilotaka kusema. Imani yetu iko katika Mungu, Mungu pekee. Tunaamini hilo.

⁴⁶ Kulikuwako na wakati ambapo maadili ya maakuli ya taifa hili yaliwekwa juu ya neno la mwanamke fulani. Ninaamini jina lake liliitwa Emily Post. Sasa, alikuwa ndiye yakini ya maadili ya maakuli. Kama Emily Post alisema, “Chukueni maharage yenu mkayale kwa kisu chenu,” lilikuwa hivyo. Humm. Hilo ndilo lenyewe, kwa sababu alikuwa ndiye yakini ya maadili ya maakuli. Kama alisema, “Kunywa kahawa yako kwa kijisahani chako, uinywe kidogo kidogo jinsi unavyoendelea,” haidhuru linasikika lisilofaa jinsi gani, lingali lilikuwa ni yakini. Kila mtu aliliheshimu kwa sababu walimchukua kuwa ndiye yakini wa maadili ya maakuli.

⁴⁷ Hatuna budi kuwa na yakini haijalishi tunafanya nini. Kama tutafanikisha lolote kamwe, hatuna budi kuwa na yakini.

⁴⁸ Kulikuwa na wakati ambapo neno la Hitler lilikuwa yakini Ujerumani. Haijalishi mtu yejote mwingine alisema nini, neno la Hitler lilikuwa ni yakini. Kama alisema, “Wafe,” wanakufa. Kama alisema, “Waishi,” wanaishi. Na kama alisema, “Twende vitani,” ama, “Hatwendi vitani,” lolote tufanyalo, neno lake lilikuwa ni yakini.

⁴⁹ Kulikuwa na wakati ambapo Italia ilikuwa na yakini. Hiyo ilikuwa ni neno la mtawala wao wa kimabavu, Mussolini, alilosema lifanywe. Walisema dereva wake alikuja kwa gari, dakika moja mapema, kumchukua. Akampiga risasi. Kwa nini? Yeye alisema, “Sikutaki hapa dakika moja mapema. Ninakutaka hapa juu ya alama, wakati hasa.” Mnaona? Neno lake lilikuwa ni yakini. Italia nzima ililiheshimu.

⁵⁰ Kulikuwa na wakati ambapo Farao, huko Misri, alikuwa ni yakini. Lakini mnaona . . .

⁵¹ Lakini maamuzi haya yote waliyofanya yalikuwa ni maamuzi yaliyofanywa na mwanadamu, na yote yakashindwa. Kwa nini? Kwa sababu hayakulingana na binadamu . . . Hayakulingana na Neno la Mungu kwa ajili ya maisha ya binadamu. Ninataka hilo, natumaini, lishike. Kama tunatarajia kuokoa maisha ya binadamu, hatuna budi kuingia kulingana na Neno la Mungu na mpango wa Mungu kwa ajili ya maisha ya binadamu. Na njia pekee utakayoupata huu, ni kuupata katika Neno Lake, na kuliamini, sasa.

⁵² Kwa hiyo, hao Mafarao. Nilikuwa huko Misri si muda mrefu uliopita, nami nafikiri iliwabidi kuchimba futi ishirini kwenda chini ardhini, kupata ma—mahali ambapo Farao aliketi kama mfalme wa dunia.

⁵³ Na Maherode wakuu, na kadhalika, tukishuka kwenye huo mstari, tunaona mahali falme zao zimeanguka na kuangamia.

⁵⁴ Bali kuna Ufalme mmoja ulio juu ya falme zote. Uko juu sana mbinguni hata kamwe hautapita. Na Huko ameketi Mfalme, ambaye, anapofanya uamuzi Wake juu ya lolote, nasi tuamini uamuzi huo, hiyo ni yakini. Utakuwa hivyo haidhuru mtu mwininge yejote anasema nini juu yake. Ndivyo ulivyo daima.

⁵⁵ Sasa, Mahakama yetu Kuu. Mahakama yetu Kuu, ni—ni yakini, mwisho wa kesi zote. Sasa, inatubidi kuwa nayo. Wakati mwininge huenda tusikubaliane na uamuzi wake. Kama vile, hawakukubaliana na wa Hitler, na kadhalika. Lakini hata hivyo hatuna budi kuwa na yakini hii. Na yakini ya taifa na kesi ni Mahakama Kuu. Mahakama zetu za mitaani zinaweza kufanyia mashtaka chochote na ziamue *hili*, bali Mahakama Kuu ina mamlaka juu ya yote. Hatuna budi kuwa nayo. Kama taifa, hatuna budi kuchukua uamuzi wake, kwa sababu taifa limefunganishwa na yakini hii ya Mahakama Kuu. Vema.

Kila kitu hakina budi kuwa na yakini.

⁵⁶ Hivi mlajua ya kwamba mchezo wa kawaida wa mpira hauna budi kuwa na yakini? Naam. Ni nini yakini ya mchezo wa mpira? Mwamuzi. Vipi kama hakuna mwamuzi, mnaona, mwamuzi? Haidhuru unasimama wapi, unaangalia mahali gami na kusema, “Ilikuwa ni mpira,” naye alisema, “Ilikuwa ni goli,” vema, hivyo ndivyo ilivyokuwa, ilikuwa goli. Kwa nini? Kwa sababu, neno lake, haidhuru watazamaji walisema nini, yale mtu mwininge yejote aliyosema. Ni goli kwa kuwa yeje alisema ni goli, naye ndiye mwamuzi. Sasa, vipi kama hakukuwako na mwamuzi? Kungekuwako na ubishi mkali mno, na kila kitu katika mchafuko, mpaka msingeweza kuwa na mchezo wa mpira. Kwa hiyo, hamna budi kuwa na yakini, mpate kuwa na mchezo wa mpira. Haina budi kuwa hivyo.

⁵⁷ Sasa, hapana budi pawe na yakini, katika taa ya trafiki. Taa ya trafiki ni yakini, hasa, kwa magari. Vipi kama hakukuwako na taa ya trafiki? Ama vipi kama taa ya trafiki ilikuwa imezima, nawe ukaenda kasi mtaani? Naye jamaa mmoja alikuwa akija *hivi*, naye akasema, “Sasa, mimi nilikuwa wa kwanza hapa. Lazima nipite pale.” Kisha kasema, “Nimechelewa kazini.” Nena kuhusu msongamano wa magari, kweli mngekuwa nao. Lakini, unaona, taa ya trafiki hulitatua. Ndiyo yakini. Ikiwa taa ni kijani, nenda. Kama ni nyekundu, simama. Iwapo hakuna kitu kama ta—taa ya trafiki, basi tungekuwa na misongamano ya magari.

⁵⁸ Na hiyo ndiyo shida katika imani ya Kikristo siku hizi. Tuna misongamano mingi mno ya magari, kila mtu akifanya yakini yao wenyewe.

⁵⁹ Wakati, tuna Yakini moja, na hiyo ni Neno la Mungu aliye hai. Hilo linalitatua milele, haidhuru mtu yejote mwininge anasema nini.

⁶⁰ Karibu imefikia mahali kama ilivyokuwa katika siku za Waamuzi, kila mtu ana yakini yao wenyewe. Lakini zote hushindwa, kama wale Mafaraao na kadhalika.

⁶¹ Bali yakini ya Mungu ni Neno Lake. Yeye hulitoa, "Na mbingu na nchi zitapita, bali Hilo halitapita kamwe." Napenda hilo.

⁶² Sasa, hatuna muda mwiningi, kwa hiyo tuangalie tu kwa dakika chache watu wachache walioingia katika matatizo, na katika nyakati ambazo mauti yaliwakabili, kama tunavyosimama usiku wa leo, nao wakachukua yakini. Hebu tuwahoji baadhi yao.

⁶³ Hebu turejee kwenye hadithi ya kale ambayo inajulikana kwetu sote, katika siku ambapo dhambi ilikuwa imelundikana ulimwenguni mpaka Mungu akakerwa na kuchoka nayo kabisa, nao ulimwengu ulikuwa unaenda kuangamizwa. Ndipo Mungu akampa Nuhu yakini, hiyo ilikuwa ni Neno Lake. Na, haidhuru, yakini hiyo ilikuwa ni ya kuwaokoa watu. Nuhu alijua ya kwamba ulimwengu ulikuwa unaenda kufa. Ndipo Mungu akampa yakini, na hiyo ilikuwa ni Neno Lake, sasa, kuwaokoa watu Wake na mauti. Sasa, yakini ilikuwa ni nini, ya kuwaokoa watu na mauti katika siku za Nuhu? Ilikuwa ni Neno la Mungu. Hiyo ilikuwa ndiyo yakini, bila kujali mtu mwininge yejote alisema nini.

⁶⁴ Yale sayansi iliyosema, "Hakuna mvua kule juu. Tunaweza kurusha zana zetu mwezini. Hakuna mvua kule. Mvua itanyeshaje?" Kama Mungu alisema kutakuwako na mvua ikinyesha, Mungu anaweza kuweka mvua angani, kama alisema hivyo.

⁶⁵ Nuhu aliendelea moja kwa moja na shughuli zake, ametulia, na kuiandaa safina kwa ajili ya kuwaokoa watu. Kwa kuwa, kulikuwa na yakini iliyotolewa kwa watu, kwamba wangeokolewa kama wakiichukua njia iliyoandalowiwa na Mungu kwa ajili ya yakini hii.

⁶⁶ Kwa hiyo, baadaye, wakati mwininge, wakati tumekubali yakini... Ningetaka kusema hili kwa sababu ya wazazi wa watoto hawa, juu ya yale ninayotaka kuwaambia katika dakika moja tu. Sasa, kama ninii... .

⁶⁷ Wakati mwininge, wakati tumelikubali, tunawekwa katika majaribu, kuona kama kweli tunaliamini. Sisi—sisi... Mungu kwa kawaida hufanya hivyo. Pia Mungu hutenda kazi... .

⁶⁸ Yeye hawezি kubadilisha mpango Wake, kwa sababu Neno Lake ni Yeye Mwenyewe. "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoa na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa kwetu. Yeye yule jana, leo, na hata milele." Kwa hiyo, daima ni Mungu.

⁶⁹ Wakati akiitwa jukwaani, kutenda kazi, na uamuzi anaofanya, Yeye hana budi kudumu na uamuzi huo daima. Hawezi kuubadilisha, kwa sababu Yeye hana kikomo.

⁷⁰ Sasa, ninaweza kubadilisha uamuzi wangu, wewe unaweza, kwa sababu tuna kikomo. Kwa hiyo, tunafanya makosa.

⁷¹ Bali Mungu hawezi kubadilisha uamuzi Wake, kwa sababu Yeye hana kikomo, na uamuzi Wa—Wake ni mkamilifu, daima. Hawezi kusema, “Nilikosea *hapa*, na nitaubadilisha uamuzi Wangu,” kwa sababu hiyo ingeonyesha Mungu angeweza kubadilika. Naye Mungu hawezi kubadilika, wala Neno Lake haliwezi kubadilika. Yeye ni yule yule, daima.

⁷² Kwa hiyo, Mungu alimpaa Nuhu jaribio, baada ya kuikubali yakini Yake. Nuhu aliiingia katika safina. Mungu akafunga mlango nyuma yake. Hapana shaka wao walisema, “Sasa, asubuhi, kutakuwako na mawingu meusi. Kisha kutakuwako na ngurumo na radi, nayo mvua itanyesha.” Lakini, mwajua, kesho yake, jua lilichomoza angavu tu kama liliyowahi kuwa.

⁷³ Ninawazia, waaminio wakwamia mpakani walisema, “Tutakwea. Mzee huyo huenda alisema kweli kuhusu hilo. Kwa hiyo, labda sayansi ilikuwa imekosea, kwamba huenda—huenda kukawa na mvua kule juu.” Lakini, kumbukeni, haikuwa imewahi kunyesha.

⁷⁴ Lakini, basi, siku ya pili, jua lilikuwa angavu tu kama liliyokuwa sikuzote; siku ya tatu, ya nne, ya tano, ya sita, na hata kufikia ya saba. Lakini Nuhu alikuwa amepanda juu kwenye chumba cha juu, kusudi aweze kuzitazama anga. Ndipo kwenye asubuhi hiyo ya saba, wakati ulipofika, ambapo watu walikuwa wameikataa njia ya yakini ya Mungu ya wokovu, ya kuyaokoa maisha ya watu, mvua ikaanza kunyesha nayo mifereji ya uchafu ikajaa. Ndipo ma—mashua ikaanza kuinuka, nayo ikampeleka Nuhu pamoja na hao kwenye usalama. Hakika, kwa sababu walikuwa wakilitumainia Neno la Mungu, ile yakini, Neno la Mungu la ahadi.

⁷⁵ Haidhuru inaonekana kuwa mbaya jinsi gani, na jinsi kunavyokuwa giza, endelea kuamini yakini yako.

⁷⁶ Musa, mbona, ninii yake, yeye alikuwa amejaribu kuyaokoa maisha ya maskini hao Waebrania. Nao walikuwa karibu wana hali mbaya, ama hali mbaya tu, kama watoto hawa wawili waliyo nayo ambaa tunajaribu kuwaokoa usiku wa leo. Walikuwa ni watumwa, nao waliwaua tu ovyo ovyo, wakati wowote waliotaka kuwaua. Basi Musa akahisi moyoni mwake ya kwamba hayo hayakuwa ni ma—mapenzi ya Mungu. Kwa hiyo, a—akajaribu kufanya hilo kwa elimu. Akajaribu kufanya hivyo kwa jitihada zake mwenyewe, na akakuta kwamba alishindwa vibaya. Alifanya jambo fulani yeye mwenyewe ambalo halikuwa sahihi, kwa sababu aliyachukua maisha ya mtu mwingine. Na hilo halikuwa sahihi.

⁷⁷ Ndipo, akaingia nyikani na akawa huko kwa muda wa miaka arobaini. Lakini, siku moja, alikuwa akiwachunga kondoo upande wa nyuma ya jangwa, na kulikuwako na Nuru kichakani. Basi Musa alipoikaribia Nuru hii, Sauti ya Mungu ikanena naye kutoka kwenye Nguzo hii ya Moto iliyokuwa huko nyuma katika kichaka hiki, na kusema, “Musa. Musa.”

Naye akasema, “Mimi hapa, Bwana.”

⁷⁸ Na Yeye akasema, “Vua viatu vyako, kwa maana mahali unaposimama ni patakatifu. Nimesikia vilio vya watu Wangu. Nimeusikia mkutano wao wa maombi. Nimekumbuka ya kwamba niliwapa ahadi.” Jamani, kama hilo halipaswi kuiwashaa moto mioyo ya waaminio Wakristo usiku wa leo! “Mimi ni Mungu. Ninakumbuka niliahidhi hili.” Jinsi hiyo Sauti ilivyokuwa ni ya Kimaandiko! Naye akasema, “Musa, ninakutuma huko chini ukawakomboe.” Ndipo Musa . . .

⁷⁹ Hakika, kama nilivyo sema hapo mwanzo, unapoichukua hiyo yakini ya Mungu, inakufanya ufanye mambo ambayo, vema, wakati mwingine ni ya kipumbavu, machoni pa watu. Ungeweza kuwazia, mtu aliyekuwa amewakimbia Wamisri, kesho yake asubuhi, baada ya kuiona yakini hii . . .

⁸⁰ Neno hili la Mungu lilisema naye ushahidi chanya, kwa sababu lilikuwa ni Neno. Ahadi ilikuwako, na thibitisho la Mungu mkuu wa maumbile, jinsi ambavyo alifanya mwujiza mbele—mbele za Musa, na kuonyesha ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu wa maumbile.

⁸¹ Naye Musa, kesho yake asubuhi, alimchukua mke wake akampandisha juu ya nyumbu, akiwa na m—mtoto nyongani mwake. Naye mwenye umri wa miaka themanini, masharubu yamenning’inia kufikia kiunoni mwake, kichwa chake chenye upara kiking’ara, ameshika fimbo iliyopinda mkononi mwake, akishuka kuelekea Misri, akipaza sauti kwa nguvu alivyoweza kwenda.

“Unaenda wapi, Musa?”

“Ninashuka kwenda Misri, kuiteka.”

“Ati kuiteka?”

⁸² Uvamizi wa mtu mmoja! Kwa nini? Alikuwa na yakini. Alikuwa na kitu fulani. Alikuwa na Neno la Mungu, angeweza kusimama juu yake. Mtu mwenye umri wa miaka themanini, akiwa na nyumbu, na fimbo mkononi mwake. Hayo ndiyo yote aliyokuwa nayo. Kama vile uvamizi wa mtu mmoja Urusi, leo hii. Lakini alishuka akaiteka, kwa sababu alikuwa na yakini. Alikuwa amezungumza na Mungu. Alikuwa ameisikia Sauti ya Mungu. Naye . . . Jambo ni kwamba, aliiteka. Kweli. Kwa nini? Hiyo ilikuwa pamoja naye siku zote za maisha yake. Ilikuwa ni yakini.

⁸³ Hakuna mtu aliye na haki kupanda mimbarani, kuhubiri Injili, isipokuwa mwenyewe amesimama kwenye mchanga huo mtakatifu, ambapo hapana kafiri wala asiyeamini anayeweza kamwe kuelezea vibaya mambo ya kimbunguni ya Mungu. Yesu asingewaruhusu wanafunzi Wake kuhubiri, hajjalishi jinsi walivyomjua vizuri; hawana budi kwenda katika mji wa Yerusalem, huko wangojee mpaka watakapovikwa Nguvu kutoka Juu. Hawana budi kupata tukio hilo.

⁸⁴ Musa, akijua ya kwamba alikuwa ni nabii, alijua alikuwa amekuzwa kwa kusudi hili, bali pasipo na huo uhusiano wa kibinagsi, hiyo Yakini, kitu ambacho kilimthibitishia ya kwamba aliposhuka kule, alikuwa anaenda kupata ukombozi kwa ajili ya watu hawa. Kamwe hakubakia yule yule. Yeye alishuka kule kwa sababu alikuwa na yakini, na akafanya yale hasa Mungu aliyomwambia afanye. Hapakuwapo na woga wowote moyoni mwake, wakati alipowatupa chini wale nyoka, ama zile fimbo, nazo zikawa nyoka. Nao waigaji wa kimwili wakaja na huduma yao, na kutupa chini na kufanya jambo lile lile. Musa alikuwa amefanya vile hasa Mungu alimwambia afanye. Hakuna chocohote cha yeye kufanya ila kusimama kimya na kuuona utukufu wa Mungu. Ndipo tunaona ya kwamba Mungu alichukua nyoka wake akala hao wengine. Hivyo ndivyo inavyofanyika. Alikuwa na hakika ya kwamba yule Mungu ambaye angeweza kumwambia kufanya hili, angeweza kumshughulikia katika hali mbaya.

⁸⁵ Hivi sisi usiku wa leo hutuwezi, juu ya msingi wa kijana mwanamume huyu kuutoa moyo wake kwa Kristo, kusimama juu ya yakini hii, kwamba Mungu anaweza kufanya yasiyowezekana yawezekekane? Anaweza kuibadilisha mioyo ya mahakimu. Kwa nini turukeruke kiwazimu sana, juu ya mambo mengine? Hebu tumchukue Mungu, kwanza. Tulirejeshe kwenye ahadi. Mungu aliliahidhi, ya kwamba—ya kwamba angefanya hilo.

⁸⁶ Kwa hiyo, kumbukeni, Musa daima alikuwa ni mtu tofauti kwa sababu alilichukua Neno la Mungu na kuliamini. Naye akathibitishiwa ahadi.

Ni wangapi tungaliweza kuwaita? Hatuna wakati.

⁸⁷ Katika kuandika muhtasari, leo hii, nilikuwa nikiandika hapa juu ya Danieli, jinsi ilivyokuwa. Illichokuwa, ilikuwa ni adhabu ya kifo kwake ku—kuomba mungu mwengine yejote. Lakini alishakuwa katika uhusiano na Mungu, naye alijua ya kwamba Mungu aliweza kumshughulikia.

⁸⁸ Wana wa Kiebrania, wangetupwa katika tanuru la moto nao wangechomwa kwa ukali wa moto, wenye joto mara saba kuliko tanuru hilo lilivyowahi kutiwa moto. Hao wana wa Kiebrania walimwamini Mungu. Wakasema, “Mungu wetu

anaweza kutukomboa na tanuru hili.” Kwa nini? Walikuwa na yakini. Walikuwa na Neno la Mungu.

⁸⁹ Naye Mungu ambaye angeweza kuwakomboa hao wana wa Kiebrania na seli ya mauti ya tanuru lililowaka moto, ni zaidi sana vipi anavyoweza kumkombo a mvulana huyu wa Kiyahudi hapa nje, aliyelala huko kwenye seli ya mauti? Ni zaidi sana vipi Yeye... Na Yeye angali ni Yehova Mungu yule yule aliyekuwa daima. Sisi, kama mtume Paulo, tunaweza kutambua ya kwamba Mungu yuyo huyo yu hai leo hii, “Jana, leo, na hata milele yeye yule.” Basi, Wakristo wanaweza kuushikilia mkono wa Mungu usiobadilika, na kubadilisha hali yote ya mambo. Maombi hubadilisha mambo. Hilo ndilo tunalotaka kufanya.

⁹⁰ Tunaweza kusema vipi kuhusu Yoshua? Atavukaje Yordani? Inaonekana kana kwamba Mungu alikuwa mwanajeshi wa kigeni, moja kwa moja katika mwezi wa Aprili, wakati maji yalipofurika namna hiyo. Lakini akamwambia Yoshua, “Lichukue sanduku usonge mbele.” Hivyo tu ndivyo ilivyompasa kufanya. Ndipo Mungu akairudisha nyuma Yordani na kufanya nchi kavu, nao wakavuka na wakaokoka. Jinsi ilivyokuwa!

⁹¹ Si ajabu Yoshua alisema, “Mimi na nyumba yangu, tutamtumikia Bwana.”

⁹² Jinsi ambavyo Daudi, yule mzee wetu mashuhuri, jinsi tungetaka kuzungumza juu yake. Hatuna wakati. Lakini, na mara nydingi... Kama tulivyomsikia mtu fulani akizungumza dakika chache zilizopita kuhusu Daudi na dhambi yake, lakini wakati yote ilisamehewa. Wakati alipokuwa akienda vitani, nasi husema, ulimwenguni, “Mambo yaliikuwa mabaya,” nao upinzani ulikuwa mkubwa. Ndipo Daudi akalala pale chini ya ule mti, akalitolea jasho, mpaka aliposikia sauti ikipitia kwenye vichaka vya miforsadi, ndipo ikawa tofauti. Daudi akasimama akaondoka, kwa sababu kwamba alikuwa na yakini, kwamba alijua huyo alikuwa ni Mungu akimtangulia.

⁹³ Hivi hatuwezi kuomba maombi ya imani ambayo yatamtuma Mungu kwenye halmashauri hiyo ya kifungo cha nje kule chini? Hakika, tunaweza. Tunaamini ya kwamba tunaweza, kama tutashikilia kwenye hiyo yakini.

⁹⁴ “Jinsi ambavyo Ibrahimu aliviita vitu, ambavyo havikuwapo, kana kwamba vilikuwapo,” kwa sababu alikuwa na ahadi ilio yakini kutoka kwa Mungu, ya kwamba Mungu atampa ninii yake... atampa mtoto kwa Sara. Hata mke alipokuwa na umri wa miaka mia moja, ama yeye alipokuwa nayo, naye mke alikuwa na tisini, “Angali hakusita kwa kutokuamini ahadi ya Mungu, bali alitiwa nguvu, akimsifu Mungu.” Nasi tunadai kuwa wana wa Ibrahimu. Wakati Ibrahimu...

⁹⁵ Wakati, tumekuwa na Biblia iliyoandikwa tangu siku za Ibrahimu, na mashahidi wote ambao tumekuwa nao

nyuma yake, kwamba Yehova hulitimiza Neno Lake, kwamba Kristo ni Mwana wa Mungu. Yeye ndiye Mpatanishi kati ya mwanadamu na Mungu, na hakuna mpatanishi mwingine kando Yake. Basi anaahidi, "Mkimwomba Baba lolote katika Jina Langu, mtapewa." Nasi tunadai kuwa watoto wa Ibrahimu. Wakati, "Ibrahimu aliiya vitu, viliyyokuwapo, kana kwamba havikuwapo, kwa sababu alimwamini Mungu." Kweli kabisa. Ninaliamini kwa moyo wangu wote.

Maisha ya Paulo yalijiyotiwa msingi katika Kristo yalikuwa ndiyo yakini yake. Yalimfunga.

⁹⁶ Kristo alikuwa ndiye yakini ya ufufuo, kama tunavyosoma hapa. Alisema, "Mungu aliapa kwa kiapo, kwa Daudi, kwamba hataiacha nafsi Yake kuzimuni." Kiapo ndicho mwisho wa ugomvi wote. "Naye aliapa ya kwamba asingeiacha nafsi Yake kuzimuni, bali angemfufua." Na kwa hiyo Yeye alimwamini Mungu, na akasulubiwa; akafa, akafufuka tena, kisha akapaa Mbinguni, kwa sababu alimwamini Mungu.

⁹⁷ Ni zaidi kiasi gani, kwa kuwa Yeye aliweka mfano, tunavyoweza kuichukua yakini hiyo! Kama Kristo aliweza kuichukua, juu ya ahadi hiyo moja pale, ni zaidi sana vipi sisi tunavyoweza kuichukua, tukiwa na maelfu ya ahadi! Na pamoja na Damu ya Yesu Kristo pale kuisafisha njia yetu, na kutuvusha lile shimo kubwa la dhambi lililotutenganisha, la kutokuamini, kutoka kwa Mungu, na kutuleta moja kwa moja katika Uwepo Wake, kuzungumza na Yeye, ni zaidi sana vipi lingweza kuwa! Naam. Hatuna budi kuwa na yakini.

⁹⁸ Ninawazia juu ya mmoja hivi sasa, katika kufunga, angekuwa ni George Washington, wakati Marekani ilipokuwa changa nasi tulikuwa tukiyapigania maisha yetu, maisha ya taifa hili kuu tulilo nalo. George Washington alikuwa ni Mkristo. Alikuwa ni mwaminio. Basi huko kwenye Bonde la Forge, ninaambibi ya kwamba majeshi ya Marekani yalikuwa tu na, ni yapata theluthi moja yao, waliokuwa wamevaa viatu. Na majira ya baridi kali yalikuwa baridi, na hali ya hewa sufuri, na mto umeganda na umevimba. Nao Waingereza upande ule mwingine. Nayo maisha ya taifa hili yalikuwa hatarini.

⁹⁹ Alifanya nini? Yeye alikuwa ni Mkristo. Anatoka nje usiku na kupiga magoti kwenye theluji, naye anaomba mpaka akalowa kwa maji ya theluji hata kiunoni mwake. Naye akakaa pale akaomba mpaka akapata ile yakini, jibu kutoka kwa Mungu, ya kwamba Mungu alikuwa anaenda kumpa ushindi.

¹⁰⁰ Ndipo kesho yake, Bonde la Forge halikuwa ni kitu kwake. Alivuka Delaware, akajisukumiza kwenye barafu pamoja na askari waliovalia nusu, wameganda nusu, miguu yao mitupu ardhini, katika theluji. Naye akastahimili, wakati risasi tatu za bunduki zilipolipenya koti lake. Kwa nini? Yeye alikuwa

akitegemea yakini ya maombi yaliyojibowi. Amina. Misingi yenye we ya taifa letu imewekwa juu ya kitu kama hicho.

¹⁰¹ Kuna shida gani na watu siku hizi wanaodai kwamba ni Wakristo? Kwa nini tunasumbuka katika saa kama hii? Hebu tuisumbuke. Hebu tuwe askari. Naam, bwana.

¹⁰² Aliomba mpaka akapata jibu hilo. Halafu, hakuna mto ulioja mawingu, hakuna askari miguu mitupu, bila kujali hali za mambo, wangeweza kuistahimili kwa sababu Mungu alikuwa amesema hivyo. Risasi hata isingaliweza kumwua, kutoka kwenye bunduki ya adui. Bila shaka. Kwa nini? Alikuwa amefanya mkutano wa maombi. Alipata jibu.

¹⁰³ Jinsi ilivyokuwa vema usiku mmoja, wakati Mtume Petro alipokuwa gerezani, nao walikuwa wamwue kesho yake asubuhi. Alikuwa afe chini ya adhabu ya kifo, kama vile maskini Myahudi huyu atakavyofanya sasa. Lakini walifanya nini? Walifanya jambo lile lile ambalo sisi hapa Houston tunajaribu kufanya. Walifanya mkutano wa maombi kwenye nyumba ya Yohana Marko. Wakati walipokuwa wakiomba, Malaika wa Bwana alienda gerezani, akazifungua nguzo za gerezani, kisha akafungua malango. Na zaidi ya hayo, akamwongoza Petro nje, naye akaja moja kwa moja kwenye huo mkutano wa maombi.

¹⁰⁴ Ninaamini, usiku wa leo, ya kwamba Mungu yuyo huyo yu hai. Iwapo Yeye si Mungu yeye yule, basi kuna kasoro fulani. Hakika.

¹⁰⁵ Ilifanywaje? Kwa mkutano wa maombi, ya Wakristo waaminifu walioamini, na waliamini ya kwamba Mungu angemkomboa ndugu yao na adhabu ya kifo. Hao walikuwa ni Wakristo waliokesha usiku kucha na kulala kifudifudi, wakalia na kuomba.

¹⁰⁶ Kama nilivyomsikia mmoja wa wahudumu, muda mfupi uliopita, akisema alikuwa anaenda kulia sana, usiku kucha. Shida yake ni kwamba, leo hii, watu wanaachilia. Wanachoka, wanashikwa na usingizi. Hata hawawezi kuketi wakamaliza ibada ya dakika kumi, ni vigumu. Vema, kuna—kuna kasoro.

¹⁰⁷ Kama unampenda Mungu, vema, vema, inatupasa kushughulika. Inapaswa kuwa ndiyo matumaini ye—yetu, shauku zetu. Inapaswa kuwa. Kila kitu kilicho ndani yetu kinapaswa kuwa katika upendo wa Kristo. Amina. Tunakaa kizembe sana. Tunakaa wasiojali sana, huku ulimwengu ukifa chini ya miguu yetu. Hiyo ni kweli. Maisha ya watu yakiondoka, bila Mungu, nasi tunaketi pasipo kujali sa—sana kulihusu. Mradi tu sisi ni wafuasi wa kanisa, hilo tu ndilo tunalofikiri kwamba linaleta tofauti.

¹⁰⁸ Nilikuwa nikizungumza juu ya Kuja kwa Kristo, majuma machache yaliyopita, katika kanisa fulani. Ndipo baadaye kulikuwako na mtu fulani aliyekutana nami nyuma ya kanisa, na kusema, “Ndugu Branham, unawashtusha watu hata kufa.”

Nikasema, “Kwa nini nifanye hivyo?”

¹⁰⁹ Akasema, “Vema, wewe kuzungumza juu ya Kuja kwa Kristo. Sitaki kusikia mambo kama hayo. Ninaye mvulana mdogo hapa sina budi kumlea. Nina msichana shuleni.”

¹¹⁰ “Loo,” nikasema, “Kuja kwa Kristo ndicho kitu adhimu sana ninachowea kuwazia.” Hakika. Mnaona?

¹¹¹ Biblia ilisema, “Wale wote *wanaopenda* kuonekana Kwake.” Loo, jamani, kwa ajili ya siku ambayo maskini mwili huu upatikanao na mauti utakapochukua kutopatikana na mauti, na hii—hii nyumba ya wadudu ninayoishi ndani yake itakapobadilishwa, katika dakika moja, kufumba na kufumbua jicho, na mwili kama mwili Wake Mwenyewe wenye utukufu! Inapaswa kuwa ndiyo shauku ya moyo wa Kanisa. Inapaswa kuwa ni kila mwanamume na mwanamke, amewaka moto, kuhubiri mitaani na kila mahali pengine, akijaribu kuwafanya watu waokoke. Bila shaka.

¹¹² Ninashangaa kama kweli tumefunganishwa kwenye yakini hiyo ambayo tunadai tumefungiwa. Hivi tunaangalia kwenye nyota sahihi ya asubuhi? Kama tunatumainia tu kanisa letu na dhehebu letu, ushirika wetu; ulimwengu unapobadilika, unabadilika pamoja na hilo, kuzunguka na kuzunguka.

¹¹³ Bali kuna Nyota moja isiyobadilika kamwe. Kuna kitu kimoja kisichowea kubadilika, hicho ni Mungu. Mungu hawezi kubadilika. Neno Lake haliwezi kubadilika. Biblia Yake haiwezi kubadilika. Na kama mtu amezaliwa kwa Roho wa Mungu, Kristo akiwa ndani yake, huitikia kila ahadi kwa “amina.” Hiyo ni kweli. Hakika.

¹¹⁴ Loo, hakika, mkutano wa maombi ndio tunaohitaji. Hatuna budi kuwa Wakristo. Wakristo wote hawana budi kutumia yakini ii hii, Neno la Mungu. Neno la Mungu ndilo msingi wa Mkristo.

¹¹⁵ Yesu alisema, katika Neno Lake, “Mkikaa ndani Yangu, Maneno Yangu yakae ndani yenu, basi mnaweza kuomba mtakayo, nanyi mtatendewa.” Wazieni hilo. Ungetaka yakini ipi zaidi? Ungetumainia nini zaidi kuliko kitu kama hicho? “Mkikaa ndani Yangu, Maneno Yangu yakae ndani yenu, basi ombeni mtakalo.”

¹¹⁶ Kumwomba Mungu atende kazi juu ya moyo wa hakimu huyo, ama halmashauri hiyo ya kifungo cha nje, na kumwachilia maskini jamaa huyo kutoka kwenye seli hiyo ya kifo! Kama tukiomba kwa imani, tukiamini, katika mikutano hii ya maombi, tutapata. Hilo, ninamwamini Mungu jinsi hiyo tu.

¹¹⁷ Na imani yangu niliyo nayo katika Mungu, hiyo ndiyo sababu nipo hapa usiku wa leo. Hiyo ndiyo sababu nilifutilia mbali jambo lingine, na kuungia hapa. Inanibidi kuendesha gari mamia ya maili usiku wa leo, kurudi Tucson, Arizona, kwa sababu nimekuja kuweka imani yangu pamoja na yenu. Huyo ni

mtu. Ni nafsi iliyolala kule. Ni mtu fulani mhitaji. Nasi Wakristo inatupasa kuzinduka tuone uhalisia, tupate imani halisi. Ifunge kwenye Neno la Mungu, na uikiri ahadi hiyo. Naam, bwana. Loo, jamani! “Mkikaa ndani Yangu, na Neno Łangu ndani yenu, ombeni mtakalo.”

¹¹⁸ Na tena, “Ikiwa watu wanaoitwa kwa Jina Łangu watakusanyika pamoja na kuomba, basi nitasikia kutoka Mbininguni.” Mkutano wa maombi, haya basi.

¹¹⁹ Ninaamini katika kuzungumza na mawakili na kuzungumza na wanasheria, ama mahakimu, ama halmashauri ya kifungo cha nje, ama chochote zaidi. Hilo ni sawa. Lakini, ndugu, kama tumaini lako halijafunganishwa na kitu ila watu wa kimwili tu wa akili, ama, akili za watu, hasa, hakika utaudhika vibaya.

¹²⁰ Lakini kama unaweza kuifunganisha imani yako kwenye mahali ambapo unajua, na ukae hapo na uombe mpaka Mungu ajibu, na unajua umelipata moyoni mwako, jambo fulani litatukia.

¹²¹ Nimeona wafu wakifufuliwa kutoka kwenye nyumba ya msiba. Nimeona ma—macho yaliyopofuka yakifunguliwa, masikio ya viziwi yakifunguliwa. Nimeona visa vya kansa tupu, pamoja na kansa ya sarkoma, ukoma, yakiponywa kwa nguvu za Mwenyezi Mungu. Kwa sababu, walikuwa na imani ya kuamini ya kwamba Mungu huyo, aliyefanya hiyo ahadi, angweza kutimiza ahadi Yake. Hiyo ni imani halisi, ya kweli kama aliyokuwa nayo Ibrahimu.

¹²² Jifunganishe hapo. Kaa hapo na uombe. Sio tu kufika pale chini, na, “Mungu, mwokoe maskini jamaa huyo mdogo na kumpeleka nyumbani.” Sote tungetaka hilo. Lakini hebu tukae hapo mpaka jambo fulani litukie. Loo! Wakati jambo fulani limetukia, basi, hakikisho hilo lingeshuka juu ya kundi hili dogo la watu walioketi kwenye jumba hili la mikutano hapa usiku wa leo, lingeshuka mionganii mwetu papa hapa, imani ya kutosha na nguvu za Mungu, kama tungeweza kuomba tufanikiwe, mpaka tuuguse huo waya wa nyumbani, mpaka ile yakini ishuke chini, Nguzo ile ile ya Moto iliyopigwa picha hapa Houston, na kamera ya Ted Kipperman, miaka kumi na miwili iliyopita. Yeye yupo hapa usiku wa leo, angali mkuu tu kama alivyokuwa wakati huo, kumkomboa mvulana huyo, ikiwa tu tutaaミニ, kwa sababu Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Ninaliamini kwa moyo wangu wote. Hiyo ndiyo sababu nipo hapa kuomba maombi yangu pamoja nanyi nyote ya kwamba Mungu atayaokoa maisha yao.

¹²³ Ndipo kama ungeweza kuomba ukafaalu, mpaka ukapata jibu, ukapata hakikisho, kama alilokuwa nalo Washington, kama alilokuwa nalo Yohana Marko, kama alilokuwa nalo Danieli, kama alilokuwa nalo Musa, mpaka umepata yakini, kitu ambacho unajua ya kwamba unaweza kujitia nanga kwake,

ndipo, "Juu ya yakini hii nitalijenga Kanisa Langu," nayo mahakama yote nchini hayawezi kuipinga Hiyo. Hiyo ni kweli. Juu ya Hiyo!

¹²⁴ Mungu yeye yule aliyeweza kumchukua maskini Myahudi kama Paulo mwenye pua iliyopinda, mwenye hasira na akishuka kule kuwaua Wakristo wote chini ya adhabu ya kifo, na angeweza kumbadilisha na kumfanya Mkristo wa kupendeza, Mungu yuyo huyo yu hai usiku wa leo, anaweza kubadilisha sheria ikawa neema, wakati wowote anapowazia kulifanya. Haleluya! Mtaniita mtakatifu anayejibingirisha, kwa vyovytovile, kwa hiyo afadhali niliingilie hilo sasa hivi. Ninamwamini Mungu huyo. Amina. Naam, bwana.

¹²⁵ Halafu Marko 11:22, wakati ulipoomba ukafaulu. Yeye alisema, "Amin, amin, nawaambia, mwaminini Mungu. Nawaambieni, mkiuambia mlima huu, 'Ng'oka.'" Wakati hiyo yakini imekuja kwako, wakati umepakwa mafuta na Roho huyo ajaye kupita udhibiti wote wa sayansi huko ng'ambo, kabla hapajakuwapo na atomu wala molekuli, Yule aliyenena kila kitu kikawa, basi wakati nafsi yako imetiwa nanga kwenye hiyo, hakuna kitu kinachoweza kuikomesha. Hiyo ni kweli. "Ukiuambia mlima huu, 'Ng'oka,' na usitie shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba ulyosema yatatimia, yatakuwa yako." Kama hiyo si yakini ya kushikilia! Hakika, ndivyo ilivyo. Hiyo ni kweli, yakini.

¹²⁶ Sasa, taifa lina yakini. Maisha yako ya nyumbani yana yakini. Kila mahali, kama kweli yatafanikisha lolote, hayana budi kuwa na yakini.

¹²⁷ Tunamthamini wakili huyu. Tunawathamini, loo, watu hao wengine wote. Kasisi huyu mzuri hapa kutoka California, na ni ujumbe mzuri jinsi gani! Na—na ndugu yetu aliyesaribu kuchukua pesa na kila kitu, kujaribu kumsaidia maskini mwanamke huyu, na—na pamoja na watoto wake, kuwaokoa. Hayo yote ni sawa. Tunathamini hilo, nami naliunga mkono.

¹²⁸ Lakini kuna jambo moja zaidi ya hilo, enyi marafiki, wakati tunapoufunga mkuutano huu usiku wa leo: Hatuna budi kulifunganisha kwenye yakini fulani, mkuutano wa maombi mbele za Mungu, ambao utatuma ukombozi kutoka kwa Yehova Mungu huyo huyo. Yeye ni Mungu tu usiku wa leo kadiri alivyokuwa wakati huo. Haleluya! Mnaamini hilo?

¹²⁹ Na tusimame kwa miguu yetu, basi, na usiku wa leo tufanye mkuutano wa maombi hapa ndani, mpaka yakini itakapotukia. Tuinue mikono yetu mbele za Mungu. Ombeni mpaka mfaulu, mpaka yakini ishuke ndani ya moyo wako.

¹³⁰ Bwana Mungu, mshushe Roho Wako Mtakatifu, na utume na uwaweke huru watoto hao huko ng'ambo, Bwana. Wameketi katika maeneo ya vivuli vya mauti. Jambo fulani liko karibu kutendeka, Bwana, nasi tunaomba ya kwamba mikutano

hii ya maombi itashika Moto. Ninakuamini Wewe, Bwana. Ninalikubali, nami ninaamini ya kwamba Wewe utawakomboa watoto hao. Tujalie, Mwenyezi Mungu. Sisi, Kanisa Lako, tunaomba hilo, kupitia Yesu Kristo. Amina. 

63-0304 Yakini
City Auditorium
Houston, Texas Marekani

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinagsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org